08

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

# TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA ZANZIBAR,

# AGOSTI, 2024

Funded by the European Union

**20 SEPTEMBA, 2024**

# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA - ZANZIBAR KWA MWEZI WA AGOSTI, 2024

## UTANGULIZI

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa kuimarisha takwimu za jinsia nchini ikiwemo kukusanya na kuchambua takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukioyaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).

## LENGO


Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia zandani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera nawatoa maamuzi.

## MATUKIO YA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA

Jumla ya matukio 157 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Agosti, 2024 ambapo waathirika walikuwa 157. Waathirika wengi walikuwa watoto sawa na asilimia 87.2, wanawake asilimia 11.5 na wanaume asilimia 1.3.


Miongoni mwa watoto (waathirika 137), wasichana walikuwa 112 (asilimia 81.8) na wavulana walikuwa 25 (asilimia 18.2).

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Waathirika wa Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, Agosti 2024**



Idadi ya Matukio ya kubaka yaliyoripotiwa yalikuwa 80, ambapo waathirika 71 walikuwa wasichana na tisa(9) walikuwa wanawake. Matukio ya kulawiti yalikuwa 14 ambapo waathirika wote walikuwa wavulana. Matukio ya kuingilia kinyume na maumbile ni saba (7) ambapo waathirika watano(5) walikuwa wasichana na wawili(2) walikuwa wanawake. Matukio ya kutorosha ni 16 ambapo waathirika 15 walikuwa wasichana na mmoja(1) alikuwa mwanamke . Matukio ya shambulio la aibu/kukashifu yalikuwa 24 kati ya hayo waathirika 15 walikuwa wasichana, manne(4) walikuwa wanawake na matano(5) walikuwa wavulana. Matukio ya shambulio yalikuwa 16 ambapo waathirika 6 walikuwa wasichana, 6 walikuwa wavulana, mawili (2) walikuwa wanawake na mawili (2) walikuwa wanaume.


**Kielelezo 1.2 Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Aina ya Matukio, Agosti, 2024**




Wilaya ya Magharibi “A” imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 38) sawa na asilimia 24.2 ikifuatia wilaya ya Magharibi “B” ambapo yameripotiwa matukio 33 (asilimia 21.0).

Wilaya ya Micheweni imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio, matukio mawili(2) yameripotiwa sawa na asilimia 1.3.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Agosti, 2024**




Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 4.8 kufikia matukio 157 mwezi wa Agosti, 2024 kutoka matukio 165 kwa mwezi wa Julai, 2024. Ambapo matukio ya kubaka yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi wa Agosti 2024.

Wilaya ya Magahribi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ikilinganishwa na wilaya nyengine (matukio 38) kwa mwezi wa Agosti, 2024 na wilaya ya Magahribi "B" iliongoza kwa mwezi wa Julai, 2024 (matukio 52).

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Julai, 2024 na Agosti, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 |
| Kaskazini 'A' | 3 | 10 | 1 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 6 | 5 | 4 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Kati | 8 | 11 | 6 | 7 | 0 | 4 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 5 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 32 | 31 | 14 | 19 | 4 | 0 | 2 | 2 | 1 | 1 | 3 | 2 | 8 | 7 |
| Magharibi 'A' | 28 | 38 | 16 | 17 | 1 | 4 | 1 | 2 | 0 | 5 | 3 | 5 | 7 | 5 |
| Magharibi 'B' | 52 | 33 | 16 | 18 | 4 | 3 | 4 | 3 | 9 | 1 | 13 | 4 | 6 | 4 |
| Wete | 8 | 5 | 1 | 3 | 4 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 7 | 2 | 5 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 12 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 | 4 | 5 | 0 | 0 |
| Mkoani | 7 | 7 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 5 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **165** | **157** | **68** | **80** | **19** | **14** | **9** | **7** | **19** | **16** | **29** | **24** | **21** | **16** |

Idadi ya matukio kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 10.3 kufikia matukio 157 kwa mwezi Agosti, 2024 kutoka matukio 175 kwa mwezi wa Agosti, 2023. Ambapo matukio ya Kubaka, Kulawiti/Kunajisi na Shambulio yameripotiwa kupungua kwa mwezi Agosti, 2024. Wilaya ya Magharibi “A” imeongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa Agosti, 2024 (matukio 38) ambapo wilaya ya Mjini iliongoza kwa mwezi wa Agosti, 2023 (matukio 50).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya na Aina ya udhalilishaji, Agosti 2023 na Agosti, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 |
| Kaskazini 'A' | 9 | 10 | 6 | 7 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 8 | 5 | 8 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kati | 10 | 11 | 4 | 7 | 3 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 4 | 3 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 50 | 31 | 21 | 19 | 7 | 0 | 0 | 2 | 2 | 1 | 5 | 2 | 15 | 7 |
| Magharibi 'A' | 29 | 38 | 12 | 17 | 4 | 4 | 2 | 2 | 0 | 5 | 1 | 5 | 10 | 5 |
| Magharibi 'B' | 36 | 33 | 11 | 18 | 5 | 3 | 2 | 3 | 3 | 1 | 5 | 4 | 10 | 4 |
| Wete | 13 | 5 | 9 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 3 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 9 | 12 | 3 | 2 | 5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 |
| Mkoani | 4 | 7 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 5 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **175** | **157** | **82** | **80** | **26** | **14** | **6** | **7** | **10** | **16** | **16** | **24** | **35** | **16** |

Miongoni mwawatoto 137 waathirika wa ukatili naudhalilishaji wa kijinsia; Wasichana waliobakwa walikuwa 71, Wavulana waliolawitiwa walikuwa 14, Kuingilia kinyume na maumbile walikuwa wasichana watano(5), Kutorosha walikuwa wasichana 18, shambulio la aibu walikuwa 16 wote ni wasichana na shambulio walikuwa 12 kati yao wasichana walikuwa 6 na wavulana walikuwa 6.

**Jadweli 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto, Wilaya na Aina ya Matukio Agosti, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 8 | 5 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Kati | 11 | 7 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 26 | 17 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 3 |
| Magharibi 'A' | 32 | 14 | 4 | 2 | 5 | 0 | 3 | 0 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 28 | 16 | 3 | 3 | 1 | 0 | 3 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 4 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 11 | 2 | 0 | 0 | 5 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Mkoani | 7 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 2 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **137** | **71** | **14** | **5** | **15** | **0** | **15** | **5** | **6** | **6** |

Miongoni mwa wanawake 18 waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia; wanawake waliobakwa walikuwa 9, kuingilia kinyume walikuwa wanawake wawili (2), Kutorosha alikuwa mwanamke mmoja(1), Shambulio la aibu/Kukashifu walikuwa wanane (4) na shambulio walikuwa wanawake wawili (2).

Jadweli 1.4a: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya Agosti, 2024

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia Kinyumena Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 5 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'A' | 5 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Magharibi 'B' | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Wete | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **18** | **9** | **2** | **1** | **4** | **2** |

Miongoni mwa wanaume wawili (2) walioripotiwa kuathirika na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, wote walifanyiwa shambulio.

**Jadweli 1.4b: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanaume kwa Wilaya Agosti, 2024**

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Magharibi 'B' | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Zanzibar** | **2** | **0** | **0** | **0** | **2** |

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 81) sawa na asilimia 59.1 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 31) sawa na asilimia 22.6. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17 (matukio 55) sawa na asilimia 77.5 kati ya matukio yote ya kubaka yalioripotiwa.

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto na Umri Agosti, 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili naUdhalilishaji | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 2 | 1 | | | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 6 |
| 6-10 | | 2 | 7 | | | 0 | 0 | 1 | 3 | 6 | 0 | 0 | 19 |
| 11-14 | | 12 | 5 | | | 3 | 0 | 3 | 1 | 3 | 3 | 1 | 31 |
| 15-17 | | 55 | 1 | | | 2 | 0 | 11 | 0 | 4 | 3 | 5 | 81 |
| **Jumla** | | **71** | **14** | | | **5** | **0** | **15** | **5** | **15** | **6** | **6** | **137** |

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Agosti, 2024 yamepungua kwa asilimia 3.5 kufikia matukio 137 kwa mwezi wa Agosti 2024 kutoka 142 kwa mwezi wa Julai 2024. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika kwenye umri wa miaka 6-10 na 15-17 yameripotiwa kuongezeka kidogo kwa mwezi wa Agosti 2024.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri, Julai 2024 na Agosti 2024**

| Miaka | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
| | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 |
| 0-5 | 2 | 2 | 4 | 1 | 2 | 0 | 1 | 0 | 5 | 3 | 0 | 0 | 14 | 6 |
| 06-10 | 5 | 2 | 6 | 7 | 1 | 0 | 0 | 1 | 6 | 9 | 0 | 0 | 18 | 19 |
| 11-14 | 14 | 12 | 8 | 5 | 1 | 3 | 3 | 3 | 4 | 4 | 7 | 4 | 37 | 31 |
| 15-17 | 42 | 55 | 0 | 1 | 4 | 2 | 14 | 11 | 5 | 4 | 8 | 8 | 73 | 81 |
| Jumla | **63** | **71** | **18** | **14** | **8** | **5** | **18** | **15** | **20** | **20** | **15** | **12** | **142** | **137** |


Idadi ya matukio ya watoto kwa mwaka yamepungua kwa asilimia 4.2 kufikia matukio 137 kwa mwezi wa Agosti 2024 kutoka matukio 143 kwa mwezi wa Agosti 2023. Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 yameripotiwa kuongezeka kwa mwezi Agosti , 2024.

**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Umri na Aina ya Matukio, Mwezi Agosti, 2023 na Agosti, 2024**

| | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Miaka | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyume na Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
| | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 |
| 0-5 | 2 | 2 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 | 0 | 0 | 9 | 6 |
| 6-10 | 5 | 2 | 9 | 7 | 1 | 0 | 0 | 1 | 4 | 9 | 4 | 0 | 23 | 19 |
| 11-14 | 15 | 12 | 8 | 5 | 1 | 3 | 3 | 3 | 2 | 4 | 9 | 4 | 38 | 31 |
| 15-17 | 51 | 55 | 2 | 1 | 3 | 2 | 7 | 11 | 1 | 4 | 9 | 8 | 73 | 81 |
| **Jumla** | **73** | **71** | **23** | **14** | **5** | **5** | **10** | **15** | **10** | **20** | **22** | **12** | **143** | **137** |

Matukio mengi (matukio 61 ) yametokea nyumbani kwa mtuhumiwa sawa na asilimia 38 . 9 ikifuatiwa na matukio yaliyotokea sehemu nyengine (matukio 48) sawa na asilimia 30.6 ikilinganishwa na maeneo mengine yaliyotajwa.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Sehemu Yaliyotokea Agosti, 2024**





Matukio 117 kati ya matukio 157 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 74.5 , matukio 35 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 22.3 ,matukio 2 yamefungwa na polisi( asilimia 1.3 ) na matukio 3 yapo mahakamani sawa na asilimia 1.9

**Jadweli 1.8: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Hatua Zilizochukuliwa Agosti, 2024**

| | | Waliofanyiwa ukatili na udhalilishaji | | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya makosa | Idadi ya makosa | Watu wazima | | Watoto | | Zilizo Mahakaman | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwa huru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Offisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi |
| | | Wanaume | Wanawake | M'me | M'ke | | | | | | |
| Kubaka | 80 | | 9 | | 71 | 1 | 0 | 0 | 2 | 23 | 54 |
| Kulawiti/Kunajis | 14 | 0 | | 14 | | 1 | 0 | 0 | 0 | 3 | 12 |
| Kuingilia kinyume na maumbile | 7 | | 2 | | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 |
| Kutorosha | 16 | 0 | 1 | 0 | 15 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 14 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 24 | 0 | 4 | 5 | 15 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 22 |
| Shambulio | 16 | 2 | 2 | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 4 | 12 |
| **Jumla** | **157** | **2** | **18** | **25** | **112** | **3** | **0** | **0** | **2** | **35** | **117** |

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Agosti 2024 walikuwa 157 kati yao, 129 walikuwa wapita njia sawa na asilimia 82.2 na jirani walikuwa 28 sawa na asilimia 17.8.

**Kielelezo 1.5: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia Agosti, 2024**



## MAJALADA YA MAKOSA YA UDHALILISHAJI YALIYOPOKELEWA AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA ZANZIBAR AGOSTI, 2024

Jumla ya Majalada 87 yamepokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwezi wa Agosti, 2024 ambayo yalihusisha makosa 90.

Idadi kubwa ya makosa yaliyopokelewa yametokea Mkoa wa Mjini Magharibi (makosa 57) sawa na asilimia 63.3 ya makosa yote ikilinganishwa na mikoa mwengine.

**Jadweli 2.1: Idadi ya Majalada na Mkosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa Agosti,2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Idadi ya Makosa |
|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 9 | 9 |
| Kusini Unguja | 7 | 7 |
| Mjini Magharibi | 56 | 57 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 3 |
| Kusini Pemba | 9 | 11 |
| Makao Makuu | 3 | 3 |
| **Jumla** | **87** | **90** |

Kati ya Majalada 87 yaliyopokelewa, majalada 17 yamependekezwa kufungwa, majalada 17 yamerudishwa Polisi kwa Upelelezi zaidi, majalada 35 yameruhusiwa kwenda mahakamani na majalada 18 hayajatolewa uamuzi.

**Jadweli 2.2: Majalada ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa na Hatua, Agosti 2024**

| Mkoa | Idadi ya Majalada | Yalio ruhusiwa kwenda Mahakamani | Yalio Pendekezwa kufungwa | Yalio rudi Polisi kwa Upelelezi | Hayajatolewa Uamuzi |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 9 | 5 | 0 | 0 | 4 |
| Kusini Unguja | 7 | 4 | 0 | 1 | 2 |
| Mjini Magharibi | 56 | 19 | 12 | 16 | 9 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 9 | 6 | 3 | 0 | 0 |
| Mkao Makuu | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 |
| **Jumla** | **87** | **35** | **17** | **17** | **18** |

Miongoni mwa makosa 90 ya udhalilishaji yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, makosa mengi zaidi yaliyojitokeza yanahusiana na kubaka (makosa 55) sawa na asilimia 61.1 ya makosa yote yaliyopokelewa.


**Jadweli 2.3: Idadi ya Makosa ya Udhalilishaji Yaliyopokelewa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa Mkoa, Agosti 2024**

| Mkoa | Idadi ya Makosa | Kubaka | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kulawiti/Kunajis | Kutorosha | Shanbulio la Aibu/Kukashifu | Kubaka kwa kundi | Kujaribu kubaka | Kurusha picha za ngongo mtandaoni | Kuteleke za mtoto |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 9 | 5 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| Kusini Unguja | 7 | 6 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini Magharibi | 57 | 39 | 2 | 7 | 2 | 6 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kaskazini Pemba | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Kusini Pemba | 11 | 4 | 0 | 1 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Makao Makuu | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **90** | **55** | **4** | **14** | **5** | **8** | **1** | **1** | **1** | **1** |

## TAKWIMU ZA UDHALILISHAJI ZILIZOFUNGULIWA KATIKA MAHKAMA ZA UDHALILISHAJI ZANZIBAR KWA MWEZI WA AGOSTI 2024

Jumla ya mashauri 32 yamefunguliwa katika mahkama za udhalilishaji kwa mwezi wa Agosti, 2024 ambapo Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na mashauri mengi yaliyofunguliwa (mashauri 22) sawa na asilimia 68.8 ikilinganishwa na mikoa mengine.

**Kielelezo 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa kwa Mkoa Agosti, 2024**




Jumla ya mashauri yaliyofunguliwa katika mahkama za udhalilishaji Zanzibar ni 32, ambapo mashauri yote 32 bado yanaendelea.

**Jadweli 3.1: Mashauri Yaliyofunguliwa katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Hatua na Aina ya Kosa Agosti, 2024**

| Aina ya Kosa | Zilizofunguliwa | Zilizotolewa uamuzi | | | Zinazoendelea |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Huru | Kufutwa | Faini | |
| Kubaka | 10 | 0 | 0 | 0 | 10 |
| Kulawiti | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Shambulio la Aibu/Kukashifu | 9 | 0 | 0 | 0 | 9 |
| Kutorosha | 5 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Kuingilia Kinyume na Maumbile | 5 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Kulawiti Mgonjwa wa Akili | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 |
| **Jumla** | **32** | **0** | **0** | **0** | **32** |

Jumla ya washtakiwa wa makosa ya vitendo vya udhalilishaji walikuwa 32 ambapo washtakiwa wote walikuwa wanaume. Washtakiwa wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 18-21 (washtakiwa 9) sawa na asilimia 28.1

Jumla ya waathirika wa vitendo vya udhalilishaji walikuwa 32 ambapo waaathirika wanne (4) walikuwa wavulana na waathirika 28 walikuwa ni wasichana na wanawake. Waathirika wengi zaidi walikuwa na umri wa miaka 10-14 (waathirika 14) sawa na asilimia 43.8.

**Jadweli 3.2: Idadi ya Washtakiwa na Waathirika wa Vitendo vya Udhalilishaji katika Mahkama za Udhalilishaji kwa Jinsi na Umri Agosti, 2024**

| Umri wa Mshtakiwa | Washtakiwa | | Umri wa Waathirika | Waathirika | |
|---|---|---|---|---|---|
| | M/ME | MKE | | M/ME | MKE |
| 14-17 | 2 | 0 | 0-4 | 0 | 7 |
| 18-21 | 9 | 0 | 5-9 | 2 | 4 |
| 22-25 | 7 | 0 | 10-14 | 2 | 12 |
| 26-29 | 2 | 0 | 15-19 | 0 | 5 |
| 30-33 | 6 | 0 | 20-24 | 0 | 0 |
| 34-37 | 1 | 0 | 25-29 | 0 | 0 |
| 38-41 | 0 | 0 | 30-34 | 0 | 0 |
| 42-45 | 1 | 0 | 35-39 | 0 | 0 |
| 46-49 | 0 | 0 | 40-49 | 0 | 0 |
| 50+ | 4 | 0 | 50+ | 0 | 0 |
| **Jumla** | **32** | **0** | **Jumla** | **4** | **28** |

## HITIMISHO

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia, muda wa matukio yalipotokea na wafanyaji wa matukio. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6). Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera na watoa maamuzi.

Jumla ya matukio 157 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Agosti, 2024 ambapo waathirika walikuwa 157. Wilaya ya Magharibi "A" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 38) sawa na asilimia 24.2. Idadi ya matukio kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 4.8 kufikia matukio 157 mwezi wa Agosti, 2024 kutoka matukio 165 kwa mwezi wa Julai, 2024.

Matukio 117 kati ya matukio 157 yameripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Jeshi la Polisi sawa na asilimia 74.5 , matukio 35 yapo Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka sawa na asilimia 22.3 ,matukio 2 yamefungwa na polisi( asilimia 1.3 ) na matukio 3 yapo mahakamani sawa na asilimia 1.9 .

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika na Aina ya Matukio Agosti, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani kwa Muathirika | 3 | [redacted] | 3 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 3 | 6 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 30 | [redacted] | 30 | [redacted] | 4 | 4 | 3 | [redacted] | 3 | 9 | 0 | 9 | 8 | 0 | 8 | 3 | 4 | 7 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 6 | [redacted] | 6 | [redacted] | 1 | 1 | 2 | [redacted] | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu za kazi | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 19 | [redacted] | 19 | [redacted] | 4 | 4 | 0 | [redacted] | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 1 | 5 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine(Vichakani na kwengine) | 22 | [redacted] | 22 | [redacted] | 5 | 5 | 2 | [redacted] | 2 | 6 | 0 | 6 | 6 | 4 | 10 | 2 | 1 | 3 |
| **Jumla** | **80** | [redacted] | **80** | [redacted] | **14** | **14** | **7** | [redacted] | **7** | **16** | **0** | **16** | **19** | **5** | **24** | **8** | **8** | **16** |

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia na Maeneo yaliyofanyika Matukio baina ya Mwezi Julai, 2024 na Agosti, 2024**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia Kinyumena Maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la Aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 |
| Nyumbani kwa Muathirika | 3 | 3 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 10 | 1 | 4 | 6 | 20 | 10 |
| Nyumbani kwa Mtuhumiwa | 27 | 30 | 4 | 4 | 5 | 3 | 9 | 9 | 5 | 8 | 6 | 7 | 56 | 61 |
| Nyumba za wageni/kwa rafiki | 3 | 6 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 6 | 9 |
| Sehemu za kazi | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Majumba mabovu | 15 | 19 | 7 | 4 | 2 | 0 | 4 | 1 | 5 | 5 | 7 | 0 | 40 | 29 |
| Sehemu nyengine(Vichakanina kwengine) | 20 | 22 | 6 | 5 | 1 | 2 | 4 | 6 | 8 | 10 | 4 | 3 | 43 | 48 |
| **Jumla** | **68** | **80** | **19** | **14** | **9** | **7** | **19** | **16** | **29** | **24** | **21** | **16** | **165** | **157** |

Jadweli 2.0: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya Agosti, 2024

| Wilaya | Idadi ya Matukio | Aina ya Ukatili na Udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 10 | 7 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 5 | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kati | 11 | 7 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 31 | 19 | 0 | 2 | 1 | 2 | 7 |
| Magharibi 'A' | 38 | 17 | 4 | 2 | 5 | 5 | 5 |
| Magharibi 'B' | 33 | 18 | 3 | 3 | 1 | 4 | 4 |
| Wete | 5 | 3 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 12 | 2 | 0 | 0 | 5 | 5 | 0 |
| Mkoani | 7 | 2 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 |
| **Zanzibar** | **157** | **80** | **14** | **7** | **16** | **24** | **16** |

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Julai, 2024 na Agosti, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 | Julai 2024 | Agosti 2024 |
| Kubaka | 68 | 80 | 5 | 9 | 63 | 71 | | | | |
| Kulawiti | 19 | 14 | | | | | 18 | 14 | 1 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 9 | 7 | 1 | 2 | 8 | 5 | | | | |
| Kutorosha | 19 | 16 | 1 | 1 | 18 | 15 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 29 | 24 | 8 | 4 | 19 | 15 | 1 | 5 | 1 | 0 |
| Shambulio | 21 | 16 | 3 | 2 | 7 | 6 | 8 | 6 | 3 | 2 |
| **Jumla** | **165** | **157** | **18** | **18** | **115** | **112** | **27** | **25** | **5** | **2** |

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Idadi ya Matukio na Waathirika wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, baina ya Mwezi Agosti, 2023 na Agosti, 2024**

| Aina ya matukio | Idadi ya Matukio | | Waathirika | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | | Wanaume | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | | | |
| | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 | Agosti 2023 | Agosti 2024 |
| Kubaka | 82 | 80 | 9 | 9 | 73 | 71 | | | | |
| Kulawiti | 26 | 14 | | | | | 23 | 14 | 3 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 7 | 1 | 2 | 5 | 5 | | | | |
| Kutorosha | 10 | 16 | 0 | 1 | 10 | 15 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 16 | 24 | 6 | 4 | 10 | 15 | 0 | 5 | 0 | 0 |
| Shambulio | 35 | 16 | 6 | 2 | 11 | 6 | 11 | 6 | 7 | 2 |
| **Jumla** | **175** | **157** | **22** | **18** | **109** | **112** | **34** | **25** | **10** | **2** |

**Jadweli 5.0: Idadi ya Waathirika Wanawake wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Agosti 2024**

| Umri | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| 18-29 | 18 | 9 | 2 | 1 | 4 | 2 |
| 30-39 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 40-49 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 50-59 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **18** | **9** | **2** | **1** | **4** | **2** |

**Jadweli 6.0: Idadi ya Waathirika Wanaume wa Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia, kwa Umri na Aina ya Matukio; Agosti 2024**

| Umri | Idadi ya Matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kulawiti | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| 18-29 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| 30-39 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 40-49 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 50-59 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 60-69 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 70-79 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 80+ | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2** | **0** | **0** | **0** | **2** |

**Jadweli 7.0: Muda wa Matukio ya Udhalilishaji Yalipotokea Agosti, 2024**

| Muda | Kubaka | Kulawiti/Kunajisi | Kuingilia Kinyume na Maumbile | Kutorosha | Shambulio la Aibu /Kukashifu | Shambulio | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 12:01 - 03:00 Asubuhi | 8 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 10 |
| 03:01 - 6:00 Mchana | 12 | 3 | 1 | 2 | 6 | 0 | 24 |
| 6:01 - 9:00 Jioni | 10 | 4 | 2 | 2 | 3 | 2 | 23 |
| 9:01 - 12:00 Jioni | 13 | 3 | 0 | 4 | 6 | 3 | 29 |
| 12:01 - 3:00 usiku | 25 | 3 | 1 | 6 | 7 | 4 | 46 |
| 3:01 - 6:00 Usiku | 7 | 0 | 3 | 1 | 1 | 5 | 17 |
| 6:01 - 09:00 Usiku | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 3 |
| 09:01 - 12:00 Asubuhi | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| **Jumla** | **80** | **14** | **7** | **16** | **24** | **16** | **157** |

## Zingatia Maelezo

Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia Kitendochochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi auya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamkekuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wangono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti,kuingilia kinyume na kimaumbile nashambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hiiya mwaka 2004. Sheria hii imetungwapamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenyeshehemu ya kumi na tatu (Section thirteen)ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendovya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyohaviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishajiwa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wakijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadikifungo cha maisha.

**Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua,2321,
Simu: +255242231869
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tzWebsite:
http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.comNukushi:
024223136
MMP, Zanzibar.